JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

**Baruapepe:ded.itigidc@singida.go.tz**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi,
01 Barabara ya Halmashauri,
S.L.P 70,
**43483 ITIGI - SINGIDA.**

Unapojibu tafadhali taja:
**Kumb. Na.** HW/ITG/F2/6/14/100

14 Januari, 2026

Kwa Wananchi Wote,
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI.**

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI LINARUDIWA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia wananchi wote wenye sifa zinazotakiwa kujaza nafasi ya kazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atakayefanya kazi katika Ofisi ya Halmashauri.

**1.0 Kazi na Majukumu ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira; -**

**1.1 Majukumu ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira**

vi. Ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri

vii. Kusimamia mchakato wa Ajira za Watumishi

viii. Watumishi na upandishaji wa vyeo Watumishi kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma.

ix. Kusimamia misingi ya haki, usawa na uwazi katika utendaji kazi wa Bodi ya Ajira hususan katika utoaji wa Ajira bila ya kushinikizwa wala kushawishiwa na chombo au Mamlaka yoyote.

x. Kupokea na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria Taratibu na Miongozo inayotolewa na Serikali kuhusu masuala ya Ajira na Bodi ya Ajira ya Halmashauri.

**1. 2 Sifa anazopaswa kuwa nazo mwombaji; -**

viii. Awe raia wa Tanzania

ix. Awe mkazi wa kudumu wa eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Itigi

x. Awe na uelewa wa kutosha katika mausala ya utawala au Menejimenti ya Rasilimali watu au Sheria/Mtumishi mstaafu aliyewahi kufanya kazi Serikalini.

Aidha mwombaji mwenye Elimu ya Shahada katika kipengele hiki atapewa kipaumbele.

xi. Awe mwadilifu na ambaye hajawahi kufungwa au kutuhumiwa adhabu yoyote kwa kosa la jinai.

xii. Umri usiopungua miaka 45 au usizidi miaka 75

xiii. Asiwe mtumishi wa Serikali, Shirika au Taasisi yoyote.

xiv. Awe na uzoefu wa kushughulikia masuala ya Utawala au menejimenti ya Rasilimali watu kwa zaidi ya miaka saba (7).

**2. 0 Maelekezo muhimu kwa waombaji;**

Kila mwombaji anatakiwa kuwasilisha barua yake ya maombi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Itigi kupitia kwa mtendaji wa kijiji na Mtendaji wa Kata katika kijiji /kata ambayo mwombaji anaishi. Aidha katika barua yake ya maombi kila mwombaji anatakiwa kuambatanisha taarifa ya maelezo binafsi (CV), cheti cha kuzaliwa, barua ya uthibitisho wa kuwa mkazi katika eneo hilo kutoka kwa Mtendaji wa Kata husika na vyeti vya shule na vya taaluma.

**3.0 Mwisho wa kupokea maombi; -**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **21 Januari, 2026 saa 9:30 Mchana**.

**4.0 Jinsi ya kutuma maombi: -**

Maombi yote yatumwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi,
**S.L.P 70,**
**ITIGI.**

Tangazo hili limetolewa na kusainiwa na.

Ayoub J. Kambi
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI